

HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P 245,
MPANDA-KATAVI.

(*Unapo jibuta fadhalii taja*):

Kumb. Na. KTV/MPDC/P.30/6/7

30 Agosti, 2017

TANGAZO LA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauriya Wilaya ya Mpimbwe, anawatangazia Wananchi wote wenye sifa za kuomba kazi za utendaji wa Kijiji Daraja la III (**VILLAGE EXECUTIVE III**)

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III – NAFASI 3

1.2 Sifa za mwombaji:

Awe na Elimu ya kidato cha nne (**Form Four**) au kidato cha sita (**form six**) aliye hitimu mafunzo ya Cheti/ Astashahada katika fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa **Hombolo**, **Dodoma** au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

1.3 Kazi na Majukumu:

- (i) Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Kijiji
- (ii) Kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango yamaendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa mikutano ya maendeleo ya Kijiji
- (v) Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (vi) kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Kijiji
- (vii) Kutunza kumbukumbu zote za uanzishwaji wa Kijiji, Mali za kijiji, rejestra za Kijiji na barua zote.
- (viii) Kuandaa taarifa za utekelezaji na kazi katika eneo la Kijiji na kuhamasisha masuala ua Uchumi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umasikini na uzalishaji mali.

- (ix) Kujibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji na Kamati ya Maendeleoya Kata.
- (x) Kupeleka, kusikiliza na kutatua migogoro ya Wananchi
- (xi) Kupanga na kuhakikisha kupitishwa kwa ratiba za vikao vya Mkutano Mkuu na Halmashauri ya Kijiji.
- (xii) Kushirikiana na Mwenyekiti wa Kijiji kuandaa Agenda za vikao mbalimbali
- (xiii) Mfuatiliaji wa miradi ya Kijiji na kutoa taarifa kwenye Halmashauri ya Kijiji.
- (ix) Kufanya lolote linalofaa kuboresha Utawala na Utendaji wa Serikali ya Kijiji.


1:4 MSHAHARA:

Kwa kuzingatia viwango vya ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS "B"

2. MAMBO YA KUZINGATIA KWA WAOMBALI

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania
2. Waambatanishe cheti cha kuzaliwa
3. Waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye Anwani na namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini.
4. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliosifika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia kazi husika.
5. **Testimonials, " Provisional Results, Statement of Results", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Sita havitakubalika.**
6. Maombi yote yatumwe kwa **Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe, S.L.P. 245, Mpanda – Katavi.**
7. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 13/09/2017 **saa 9:30 Alasiri**

LIMETOLEWA NA:



.....
Erasto N Kiwale,

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE.**


MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) MPIMBWE